

MANENO YAKE YA

AHADI YASIYOSHINDWA

 Kusudi sote tuweze kuingia katika hali ya kuwaombea wagonjwa. Na sasa tunataka pia kuwa katika maombi kwa ajili ya mkutano ujao wa Wafanyabiashara hapa, unaoanza Alhamisi ijayo jioni. Watakuwa na wahubiri wazuri katika huu mku-. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

² Tucson, hakika, naishi Tucson sasa. Huu ni mwaka wangu wa pili huko. Na kama ambavyo nimesema daima, “Ninaishi Yerusalemu.”

³ Nisingeweza kuwa polisi (jana usiku walinipa ti—tikiti) nikiamini kwamba huo ulikuwa ni Yerusalemu. Nilikuwa njiani nikienda huku juu karibu na Makutano ya Apache, ndipo moja ya taa zangu ikazimika, taa ya mbele, taa ya kuashiria. Nami nilikuwa ninajaribu kufika kwenye kituo cha petroli, ndipo nyingine ikazimika. Na ilitokea kwamba nilitazama nyuma yangu, ndipo nikaona taa yake nyekundu. Akanisimamisha, naye akasema, “Unajua nilichokusimamishia?”

Nikasema, “Naam, bwana, taa moja imezimika.”

Akasema, “Hiyo ni kweli. Unajua ni ukiukaji sheria kufanya hivyo?”

⁴ Nikasema, “Naam, bwana, lakini ni—ni—nisingeweza kufika kwenye kituo. Sikupata chochote. Nilikuwa najaribu kutafuta kimoja.”

Akasema, “Unatoka wapi?”

Nikasema, “Yerusalemu.”

Akasema, “Ati wapi? Wapi?”

Nikasema, “Yerusalemu.” Nikasema, “Mimi ni. . .”

Akaiangalia leseni yangu, kasema, “Wewe ni mhudumu?”

Nikasema, “Naam, bwana.” Nikasema, “Ninatoka Yerusalemu.”

Kasema, “Huko ni wapi, ng’ambo ya bahari?”

⁵ Nikasema, “La, bwana. Uko juu ya kilima hapa, unaoitwa Tucson, mnauita hivyo.” Nikasema, “Nimekuwa huku chini Yeriko, hapa, nikihudumu kwenye bonde.”

⁶ Ni ajabu hakunipa tikiti wakati huo basi, sivyo? Lakini a—alinipa ki—kidogo, “Harakisha ukaitengeneze, au. . .” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁷ Bwana Yesu, tunajikabidhi Kwako, kwa ajili ya ibada hii. Ninayakumbuka mambo yote ambayo Wewe umeniambia, na mambo yote ambayo Wewe umefanya mbele za watu, kwa hili tunakupua sifa na utukufu. Lakini nakumbuka msimu wa kupukutika uliopita, nikishuka, yapata maili mia tano kaskazini mwa hapa, wakati uliponionyesha mlima ule, na kusema, “Rudi ukawaombe watu wagonjwa, mpaka wakati utakapotimia.” Nami huyu hapa, Bwana. Si kwa ajili ya watu hawa hapa; siwaombi wao. Ninakuomba Wewe. Nami nipo hapa usiku wa leo katika huduma Yako, kufanya tu jinsi unavyoniagiza. Nisaidie sasa, Baba, ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

⁸ Hebu tugeukie katika Biblia sasa, kwenye, Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, kwa ajili ya fungu. Na hebu tusome Mathayo Mtakatifu, mlango wa 24, na kifungu cha 32 na 35, vyote pamoja.

Basi kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake likiisha kuchipuka na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu;

Nanyi kadhalika, myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu karibu, milangoni.

Amin nawaambia, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatakapotimia.

Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe.

⁹ Ningependa kuchukua somo dogo kutoka hapo, juu ya hili, *Maneno Yake Ya Ahadi Yasiyoshindwa*. Imani yetu imewekewa msingi papa *Hapa*, juu ya Neno la ahadi lisiloshindwa. Mwanadamu, kupitia nyakati, ametumaini Hili, katika ahadi za Mungu.

¹⁰ Sasa, kama uliwahi wakati wowote, maishani mwako, kuja kwenye ibada ya uponyaji, na ulitaka kusikiza kwa makini uwezavyo, ninataka yafanye hivyo sasa. Tunataka kumwona Bwana akitukuzwa.

¹¹ Nami kwa kweli ninaamini kwamba kila Neno la Mungu, kila ahadi aliyofanya, ni kweli.

¹² Nalo ni kwa kila mtu atakayelikubali. Na sasa kuna wengine ambao hujaribu kulikubali, nao hawawezi. Kuna wengine wanaoweza kulipokea. Na wengine wanalipata bila kujaribu hata kidogo. Sasa, hilo, inatubidi kuhubiri Injili kwamba “uponyaji ni kwa wote,” hata hivyo tunajua sivyo ulivyo. Ni kwa wote kama wanaweza kuupokea, bali tunajua kwamba wote hawawezi kuupokea. Ninataka tu kuwa mwaminifu kwenu kadri niyuavyo.

¹³ Inatubidi kuhubiri wokovu kwa njia iyo hiyo, kwamba “wokovu ni kwa ajili ya wote,” bali tunajua kwamba wote hawawezi kuupokea. Watu wote hawawezi kuona mambo haya.

Yesu alisema, “Heri macho yenu yawezayo kuona, ufahamu wenu, kwa kuwa kuna wengi wasioweza kulifahamu.”

14 Nao uponyaji wa Kiungu ni kwa ajili ya wale wanaoamini. Bali, huwezi kuamini mpaka Kitu fulani kiwe ndani yako, kukufanya uamini.

15 “Na tena kama kazi zingalifanywa,” Yesu alisema “Sodoma na Gomora, zilizofanywa katika miji ya Kapernaumu na miji hiyo” aliyokuwa ameipitia, Yeye alisema, “ingekuwa imesimama hadi wa leo.”

16 Nami ninasema: Kama kazi, kazi kuu ambazo zimefanywa Phoenix, zingalifanywa Sodoma, ungebakia mpaka leo hii, wala usingekuwa chini ya Chumvi . . . ya Bahari ya Chumvi.

17 Sasa, ni kwa sababu kwamba watu wote wanaukimbilia, wote walio wagonjwa. Lakini laiti wangalisimama tu kwa dakika moja, na kujaribu kufikiria kile Neno linachomaanisha.

18 Imani ni kwa kusikia Neno, Neno la ahadi. Ikiwa huna ahadi, basi unajasiria kwa msingi wa imani yako mwenyewe. Bali, ikiwa unaweza kuchukua ahadi ya Mungu, hiyo ni ahadi ya Mungu kwako.

19 Yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, hakuwa na ahadi ya hilo. Lakini imani yake, pasipo na ahadi, ilimpa uponyaji.

20 Sasa, kama aliweza kupata uponyaji wake, kwa imani yake, bila ya ahadi katika kile alichokuwa akifanya, ni zaidi sana jinsi gani tunapaswa kupokea uponyaji wetu, kwa imani katika ahadi ambayo Mungu anadhihirisha na kuthibitisha mbele zetu, na ametuletea kwa Neno Lake, akaja na kulithibitisha Neno Lake!

21 Waangalie watoto hawa wachanga ambao ndio kwanza niwaweke wakfu. Wote wawili, muujiza kutoka kwa Mungu, imepita ufahamu wa matibabu. Mnaona? Wazia tu mambo ambayo yamefanywa!

22 Sasa, je! Mungu ana upendeleo? Bila shaka sivyo. Kama akimponya mmoja, atamponya huyo mwingine. Lipo jambo moja tu likupasalo kutenda, ni kuitumia imani hiyo. Nayo imani hiyo ni kitu unachokijua; si kitu unachoingilia ghafula, kubahatisha. Unaijua! Jambo fulani linatukia. Sasa, kote katika nyakati, watu wameegemea kwenye hili.

23 Sababu yangu ya kuchukua fungu hili hapa kwa dakika hizi chache, ni kwa sababu Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe.” Naye alikuwa amefanya ahadi hapa, kwamba kizazi hicho, wangeninii . . . Kasema, “Kizazi hiki hakitapita hata mambo haya yote yatimie.”

24 Kama kungetokea kuwa na asiyeamini aliyeketi hapa, hilo ndilo moja ya mawe makuu zaidi ya kujikwaa ambalo asiyeamini alipata kujikuta ndani yake. Wanafikiri kwamba Yesu alikuwa

akirejelea kile kizazi alichokuwa akikizungumzia. Sasa ili kunyosha jambo hilo, kusudi tuweze kulifikia somo.

²⁵ Walimwuliza maswali matatu. Kama utatambua huko nyuma katika wa 24, mwanzo wa mlango wa 24 hapa, tunasoma Maneno haya.

Yesu akaenda zake, akatoka hekaluni; wanafunzi wake wakamwendea . . . ili kumwonyesha majengo ya hekalu.

Naye Yesu akajibu akawaambia, Hamyaoni haya yote? Amin, nawaambieni, Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomoshwa.

²⁶ Sasa, hapo ni wakati Yeye alikuwa angali jijini, kwenye hekalu. Sasa kitu gani?

Hata alipokuwa ameketi katika mlima . . .

²⁷ Aliondoka kutoka hekaluni, akapanda juu ya mlima, Mlima wa Mizeituni.

. . . akaketi juu . . . Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamwendea kwa faragha, wakisema, Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? . . . ni nini dalili ya kuja kwako, na dalili ya mwisho wa dunia?

²⁸ Walimwuliza maswali matatu, na Yeye anawajibu jinsi walivyomwuliza. Maswali matatu, mnaona. Kwanza, “Ni lini kutakuwapo wakati jiwe moja halitasalia juu ya jingine?” Na, “Ni nini itakayokuwa dalili ya Kuja Kwako?” Na, “Ni nini mwisho wa dunia?” Maswali matatu. Naye anayajibu maswali matatu.

²⁹ Wanafunzi mashuhuri, leo hii, wanaweka swali hilo la kwanza, wakati Yeye aliposema, “Ombeni kwamba kukimbia kwenu kusiwe ni wakati wa baridi, wala siku ya sabato,” wanaweka hilo katika siku za usoni, la Kuja kwa Bwana katika mwisho wa dunia.

³⁰ Hilo lilitendeka katika A.D. 70, wakati askari mkuu wa Kirumi, ama jeshi kuu, Tito na kundi lake walipopanda kule, yule jemadari mkuu wa Rumi, walipozunguka kuta kama Yesu alivyokuwa amewatabiria. “Na mkiona Yerusalemu imezungukwa na majeshi, basi yeye aliye kondeni na asirudi mjini tena.” Sasa ingefaidi nini . . .

³¹ Na watu wengine wanajaribu kutetea fundisho lao juu ya hilo, kwamba watu watakuwa wangali wanaishi katika majira ya sabato, wakilinda siku za sabato, wakati Yeye atakapokuja. Vema, kama ninii—kama Kuja huko ni kwa ulimwengu wote, usingekuwa unalinda sabato; kwa kuwa, sehemu moja, ni siku ya sabato, na siku inayofuata ni siku baada ya sabato. Mnaona, kwa hiyo sivyo. Kulinda sabato kulikuwa ni kwa ajili ya watu nyikani, si kwa Kanisa la ulimwenguni kote. Mnaona? Na mambo haya yote mbalimbali, wanachukua hayo Maandiko

pasipo kuwa na Roho Mtakatifu kuyagawanya sawasawa na kuonyesha kile yalicho.

³² Lakini hili hapa kile Yesu alikuwa akinena, kwa maoni yangu manyenyekevu kabisa, ni kwamba Yeye alisema, kwamba, “Kizazi hiki,” kwa maneno mengine, “kile kizazi kilichoonna mtini ukichipuka.” Mnaona, Yeye alisema hapa, “Basi mtini unapoanza, ni mchanga, na unachipusha ninii yake, matawi yake, mwasema wakati wa mavuno umekaribia. Vivyo hivyo, mnaona, mnapoona mambo haya yote, mnajua wakati. Mtakapoona maswali haya yote matatu yakitimia, wakati umekaribia. Kizazi hicho kitakachoonna huo mtini!” Nao *mtini* daima ni “Israeli.” “Na wakati Israeli inaporudi kwa nchi ya wenyeji wake na kuwa taifa, kizazi hicho hakitapita mpaka mambo haya yote yametimia.”

³³ Basi Wakristo wapendwa, usiku wa leo, katika mchafuko huu mkubwa kwenye Maandiko, ambapo watu wanafikiri yamechanganyana, sasa tunaishi kuona ninii hasa. . . Kila kitu ambacho alisema hapa kimetimia, kitu tu kinachofuata ni kwa ajili ya Kuja Kwake.

³⁴ Israeli iko katika nchi ya wenyeji wake. Imekuwa taifa huru. Ina pesa yake, bendera yake, mshirika wa U.N. Ni taifa tu; kwa mara ya kwanza, kwa yapata miaka elfu mbili mia tano, tangu imekuwa taifa. Na Yesu aliahidi kwamba, “Kizazi kile. . .” Pia, katika Biblia, kizazi kimetengewa miaka arobaini. Kuanzia wakati ambapo Israeli ilifanyika taifa, hadi miaka arobaini, mahali fulani katika kipindi hicho, Yeye atakuja. Na kama hiyo ni kweli, basi hiyo inaleta Kuja.

³⁵ Vema, na kitu kingine, kila miaka elfu mbili, jambo fulani limetukia duniani, na siasa na kila kitu kutolewa, ilibidi Mungu atume msaada kutoka Mbinguni. Na miaka elfu mbili ya kwanza, dunia iliharibiwa kwa maji; miaka elfu mbili ya pili, Kristo akaja; na huu ni 1964, nao wanadai kwamba tuko miaka kumi na saba nyuma katika huo.

³⁶ Sasa mnaona kuko mlangoni. Jambo linalofuata, ni, kutazamia Kuja kwa Bwana. Dalili zingine zote zinaingiana moja kwa moja nalo. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu, usiku wa leo, kwamba ninajaribu kuwafanya watu wakae moja kwa moja kwenye Neno lililoahidiwa. Kile tu Neno lisemacho, kaa moja kwa moja na Hicho.

³⁷ Sasa, nilipomjia Kristo, nilijua ilinibidi kuwa na msingi mahali fulani, kusimamia. Niliwekwa wakfu katika kanisa la Baptisti ya Kimishenari. Ndipo nilipoona mafundisho ya kanisa la Baptisti ya Kimishenari yalikuwa kinyume sana na Maandiko, basi nisingeweza kuweka, kugemeza matumaini yangu kwenye mafundisho ya kanisa la Baptisti ya Kimishenari. Basi nikawazia ningeenda kwenye kanisa la mama yangu, alikuwa Methodist. Nami nikawazia ningeenda huko. Nikapata

tena. Kwa hiyo nilijua kwamba Yesu akiwajia watu wa Methodist, hakika angewaacha nje Wabaptisti. Kama akiwajia Wabaptisti, angewaacha Wamethodisti. Lakini nikaona, katika makundi yote mawili, watu wazuri. Nami nikajua kwamba kama akilijia kanisa, angelijia kanisa gani, madhehebu mbalimbali mia tisa na kitu? Halijii kanisa. Yeye hatawahukumu watu kwa kanisa.

³⁸ Anaenda kuwahukumu watu kwa Yesu Kristo. Naye Yesu Kristo ni Neno. Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, ilisema, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno.” Wakati Mungu... Hapo mwanzo, kabla ya kuwa Neno, lilikuwa ni wazo. “Ndipo basi hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Lote lilikuwa ni Mungu.

³⁹ Ndipo basi Mungu alipolitoa Neno Lake, kile kingekuwa, alichagua Kanisa Lake kimbele, kabla ya msingi wa dunia, “Lingeonekana mbele Zake, bila waa wala kunyanzi.” Nayo saa inasonga moja kwa moja. Na Hilo litakuwapo, Kanisa, Kanisa tukufu, bila waa wala kunyanzi! Ninatumaini ya kwamba sisi sote, hapa usiku wa leo, ni washiriki wa Kanisa hilo. Na kwamba kuna njia moja tu ya kuingia Kanisa hilo, si kwa dhehebu lolote, unaingia Hilo kwa kuzaliwa upya.

Nawe unasema, “Vema, ninaamini hilo.”

⁴⁰ Na kama unaamini, basi utaitikia kila Neno la Biblia hii, kwa “amina,” kila kitu Biblia isemacho; kwa sababu Hiyo ni Kristo, na wewe ni sehemu ya Kristo, na Roho Mtakatifu akifunua Kweli hii. Kila wakati umekuwa na sehemu yake ya Neno la kutimizwa.

⁴¹ Mungu daima humtuma nabii. Neno humjia nabii; Neno lililoandikwa, tambuzi la mawazo ya moyoni. Ulitambua hilo wakati wote? Nabii, kwa kuwa alijua kwamba yeye alikuwa ni nabii, ni kwa sababu kwamba Neno la Mungu hutambua wazo lililoko moyoni, hutabiri mambo, msema kimbele na mtabiri. Je! uliwahi kuchukua kamusi, kamusi ya kale ya Kiebrania, na kuona kile neno *Mwonaji* linamaanisha? Ni yule aliye na ufunuo wa Kiungu wa Neno lililoandikwa. Na jinsi linavyothibitishwa, yeye huona mambo kimbele anayotabiri, nayo yanatimia.

⁴² Sasa, hiyo inafananaje na Maandiko? Hakika kabisa. “Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake, kuna naye katika maono. Na mambo haya yakitimia, basi ni Mungu. Yasipotimia, basi msimsikie; msimwogope hata kidogo, bali mlipuuze tu.” Lakini Neno la Mungu daima ni kweli! Hivyo basi, hivyo ndivyo walivyomjua mtu aliyekuwa akizungumza, kama alikuwa na ufunuo wa kweli wa Neno, au la, Neno la Kiungu lililoandikwa, ni kwa sababu alikuwa na Neno la Bwana likimjia. Sasa tunakaa Hapo, tunajiweka wenyewe na tumaini letu juu ya Neno hili.

⁴³ Unasema, “Ndugu Branham, katika Agano la Kale, hao walikuwa ni manabii.”

⁴⁴ Mungu, katika Biblia, Waebrania, mlango wa kwanza, ilisema, “Mungu, zamani za kale, katika njia mbalimbali alinena na baba zetu kupitia manabii; katika siku hii ya mwisho amenena kupitia Mwanawe, Yesu Kristo.” Mnaona, ni Yesu Kristo. Na Yesu ni Neno, mnaona, na hufunua Neno Lake kwa Yesu Kristo. Neno hujifunua Lenyewe, hufanya Neno kuishi. Hapo ndipo watu wanapokosa kumtambua.

⁴⁵ Hivyo ndivyo maskini yule mwanamke, kisimani, alivyomtambua. Mbona, alijua, upesi. Punde tu alipomwambia huyo mwanamke jambo lililomhusu mwenyewe, mwanamke huyo akasema, “Bwana, natambua Wewe ni nabii. Sasa, tunajua Masihi yuaja. Na ajapo, Yeye atatuambia mambo haya, atuonyeshe mambo yote.”

Akasema, “Mimi Ndiye ninayezungumza na wewe.”

⁴⁶ Angewezae kukana madai Yake, wakati kazi ilifanywa kwanza? Kazi ilithibitishwa kwanza, kwamba Yeye alikuwa ni yule Nabii. Hawakuwa wamekuwa na manabii kwa mamia ya miaka. Na Mtu huyu ilibidi awe ni nabii; na—na akisema, kwa kujithibitisha Mwenyewe, kwamba Yeye alikuwa ni yule Masihi aliyeahidiwa. Si ajabu maskini yule mwanamke angeweza kukimbia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Haimkini huyu kuwa ndiye Masihi, Masihi mwenyewe?”

⁴⁷ Sasa tunaamini kwamba, kwamba Mungu, katika nyakati ambazo amezigawia Neno Lake, kundi hilo, Neno hilo litafunuliwa katika Kweli Yake. Litathibitishwa, kwa sababu Mungu aliliahidi hivyo. Nalo, ni, ni kweli daima.

⁴⁸ Nuhu. Ilikuwa vigumu kwa watu kumwelewa Nuhu katika siku zake. Alimsikia Mungu akinena. Alijua lilikuwa ni Neno, kwa sababu alikuwa ni nabii wa Mungu. Mungu alimtuma, kutangaza, “Gharika kuu inakuja!” Aliijenga safina, katika wakati wa pingamizi. Haikuleta tofauti yoyote kwa Nuhu, ni wangapi waliopinga. Alikuwa ndiye nuru ya siku hiyo. Alikuwa ndiye Neno la Mungu lililodhihirishwa kwa ajili ya siku hiyo; kwani, Mungu aliwaangamiza watu.

⁴⁹ Musa, mwanatheolojia mashuhuri, mwenye akili, mtu mashuhuri, aliyezaliwa kuwa nabii; hata hivyo, katika theolojia yake yote na ninii yake—maarifa yake ya kitabu kumhusu Mungu, asingeweza kuwakomboa wana wa Israeli kwa maarifa.

⁵⁰ Mnaona, nabii hawezi kuenenda kwa maarifa. Inambidi kwenda kwa uvuvio. Uvuvio!

⁵¹ Ndipo wakati Neno la Bwana lilipomjia nyikani, katika kichaka kilichowaka moto, na kumwambia na kumfunulia Maneno ambayo Yeye alikuwa amenena kwa Ibrahimu. Basi Yeye

alikuwa anafanya nini? Kumwonyesha Neno lililoandikwa la wakati huo, na kisha akamwita Musa kwa ajili ya kazi. Naye aliogopa, pamoja na jeshi, kujaribu kuikomboa Israeli; na kisha anashuka kwenda na kijiti mkononi mwake, na anaikomboa Israeli. Ninii—ninii. . .

⁵² Mungu hulifanya kisiri sana, ambalo huifanya nia ya kimwili kupoteza mwelekeo. Haiwezi kuwaza tena. Hivi uliwahi kutambua?

⁵³ Yohana Mbatizaji, akisimama majini, yeye alikuwa ni nabii, mtangulizi, kati ya manabii na kuja kwa Mwana wa Mungu. Yohana alitembea akaingia majini, ndipo akasema! Hakuogopa kuwaambia watu, “Amesimama Mtu miongoni mweni sasa!” Hebu wazia tu kuhusu hakikisho alilokuwa nalo! “Amesimama Mmoja miongoni mweni sasa hivi, ambaye hamumjui. Viatu vyake sistahili kuvibeba. Atakuwa ndiye Yule ambaye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.”

⁵⁴ Alikuwa katikati ya watu wakati huo. Yohana alijua ilimbidi Yeye kuja katika kizazi chake, kwa sababu aliona mahali pake katika Maandiko, akaona Roho wa Mungu juu Yake. “Namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuitengeneza njia.” Naye alijua kule kuja kwa Masihi kulikuwa kumekaribia.

⁵⁵ Kwa hiyo wakati nabii alipokuwa amesimama ndani ya maji, akitabiri, Neno lilimjia. Yesu alikuwa ni Neno! Hivyo ndivyo nabii alivyomjua, kwa sababu ilikuwa ni Neno, pamoja na ishara aliyokuwa amepewa. “Nilimjua, kwa sababu Yeye aliyeniambia, nyikani, ‘Nenda, ukabatize kwa maji,’ alisema, ‘Yule utakayemwona Roho akishuka juu Yake, na kutulia, Huyo atabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.’” Na wakati Neno lilipokuja, ishara ilikuja pamoja na Neno, ndani ya maji.

⁵⁶ Yesu Mwenyewe, wakati alipokuja, alijua Yeye alikuwa ni Neno. Yeye, Yeye alikuwa na hakika na hilo. Kwa sababu, Yeye, wakati alipokuwa tu na umri wa miaka kumi na miwili, Mvulana mdogo, tunamwona Yeye (kama nilivyokuwa nikinena jana) ndani ya hekalu, akibishana na makuhani. Maarifa Yake yanguweza kupita mapokeo yao, na Yeye alikuwa akiwafundisha, hao wanaume. Ndipo wakati mama Yake Mwenyewe alipomjia, na kufanya. . .kusema neno ambalo halikuwa sahihi, tazama Neno likisahihisha kosa.

⁵⁷ Neno daima husahihisha kosa. Na iwapo watu wangeweza tu kuliona leo hii, Neno husahihisha kosa! Kitu chote kinakuwa ni kosa. Ila Neno la Mungu ndilo lililo sahihi. Yeye alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita.”

⁵⁸ Nalo Neno lililotabiriwa kwa ajili ya siku hii, husahihisha kosa la siku hii. Mnaelewa? Neno Lenyewe husahihisha kosa. Watu leo hii, wanasema “Loo, hebu tujiunge na *hili*. Hebu tuende kwenye Baraza. Hebu tufanye mambo *haya* yote.” Hilo ni kosa. Basi Neno hurudi na kusahihisha kosa hilo, kwa kujitambulisha

Lenyewe, wakati, na majira ya wakati. Sasa tunajua mambo hayo ni kweli.

⁵⁹ Sasa ninaenda kuwapa ushuhuda mdogo wa kibinafsi katika dakika kumi zijazo, Bwana akipenda, ushuhuda mdogo wa kibinafsi. Ambao, ninaamini, kama sijakosea, Ndugu John Sharrit...Sijui kama yuko humu jengoni usiku wa leo, au hayuko. Sijamwona. Yeye ni rafiki wa karibu sana, ndugu wa thamani. Alikuwa pamoja nami katika sehemu ya mwanzoni mwa huduma.

⁶⁰ Ni wangapi waliokuwa hapa wakati nilipokuja Phoenix mara ya kwanza, miaka kumi na sita iliyopita? Hebu tuone mikono yenu. Angalia tu pale, kwa kweli theluthi moja ya watu. Ni wangapi wenu wanaokumbuka kwamba, katika kuwaombea wagonjwa, ningenyosha mkono wangu, watu wangeweka mikono yao juu ya—juu yangu; na kisha, lolote lililonenwa, ndilo walilokuwa nalo. Ni wangapi wanakumbuka hilo?

⁶¹ Na wangapi wenu wanakumbuka kwamba niliwaambia kwamba Malaika wa Bwana, katika ile Nguzo ya Moto, aliye—aliyekutana nami kule juu, na kuniambia, kama “ningekuwa mwaminifu,” ingetimia kuwa “ningejua siri zenyewe za moyo.” Ni wangapi wanakumbuka hilo, alisema ingekuwa hivyo?

⁶² Sasa, ni wangapi wanaokumbuka kwamba Yeye aliahidi kwamba ingeendelea? Na, si muda mrefu uliopita, kwa ajili ya ono, Yeye aliahidi kuhusu ule mvuto wa ule ugwe, kasema, “Huwezi kuwafundisha watoto wachanga wa Kipentekoste mambo ya kimbinguni.” Ndipo nilipofanya mvuto wa tatu, Yeye alisema, “Sasa usimwambie yeyote kuhusu huu. Umekuwa ukijaribu kueleza ule mwingine. Usimwambie yeyote kuhusu huu. Huu ndio mvuto mkuu na wa mwisho.” Ni wangapi wanaokumbuka hilo kubashiriwa?

⁶³ Mnaona, Yeye kamwe hashindwi. Mambo hayo yalitendeka, moja, mbili, tatu, kama tu yalivyokuwa.

⁶⁴ Sasa, katika Phoenix, huo ulikuwa ni wakati ambapo Bibi Waldroff hapa alikuwa amefariki kwenye mstari wa maombi, akiwa na kansa moyoni mwake, naye akaponywa. Yeye huja mikutanoni kwa kawaida. Labda yupo hapa sasa. Na kisha... Bibi Hattie Waldroff. Ndipo tunapata ya kwamba daktari wake alikuwa na ushuhuda wa jambo hilo, akatoa pi—picha, au si ninii...Zinaitwaje, eksirei? Eksirei zake, ambapo mwa—mwanamke huyo alikuwa na kansa. Naye anaishi leo. Na hiyo ilikuwa ni miaka kumi na sita iliyopita. Sasa nina hakika kabisa ya kwamba bwana...Naam, yule pale Bibi Waldroff, pale pale sasa. Hiyo ni kweli. [Mtu fulani anasema, “Hiyo imekuwa ni miaka kumi na saba, hii Machi.”—Mh.] Hiyo ni miaka kumi na saba, hii Machi. Huyu hapo mama aliyekufa, na akafufuka tena, akiwa na kansa moyoni mwake. Kwa sababu, ilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa angalia nyakati hizo.

65 Nilienda California, nami ninaamini kwamba Ndugu John Sharrit alikuwa pamoja nami wakati huo. Nilikuwa nikiwazia leo, nikiwaza kuhusu hilo, nikija huku. Nina hakika kabisa alikuwa pamoja nami. Basi mimi na mke wangu. . . Na Rebeka wangu, mwanamke kijana sasa, anahitimu mwaka huu; alikuwa ni mtoto mchanga, nilikuwa nimembeba kwenye mikono yangu. Na tulienda, pia, tulienda Catalina, tulikuwa tukienda Catalina baada ya mkutano kumalizika, tunachukua tu mtumbwi na kurudi, ili tu kusema tulikuwa baharini. Na usiku kabla hatujaondoka, ama siku moja ama mbili usiku. . .

66 Paul Melikian, karibu ninyi nyote mnamjua. Paul Melikian. Ninaamini yuko pamoja na ta-. . . Nini? [Ndugu mmoja anasema, “Madera.”—Mh.] Wapi? [“Madera.”] Madera, California. Mama yake, baba, wote wawili walikuwa wameponywa kwenye mikutano. Niliruka huku kwa ndege, kuwatembelea, nao wakaponywa.

67 Mke wa Paul alikuwa ndiyo kwanza ajifungue m—mtoto. Watu wazuri, Waarmenia, nao walipiga simu kule chini na kuuliza, mke alikuwa mgonjwa na alitaka kumleta. Nikasema, “Vema, njoo huku chini.” Kwa hiyo, wakamleta huko chini. Basi usiku huo. . . Yeye, na mke wangu pamoja na mimi, na huenda ikawa ni Ndugu Sharrit. Sina hakika.

68 Je! Ndugu Sharrit yupo hapa? Kama angekuwa. . . Hiyo ilikuwa kweli, Ndugu Sharrit, ulikuwa huko usiku huo? Hiyo ni kweli. Huyu hapo shahidi. Ni—nilikuwa nikitafuta kumwona Ndugu John, na kuona kama alikuwa hapa.

69 Sasa yeye aliweka mkono wake juu ya wangu, na upesi ukavuma. “Basi, angalia, ana uhai wa kumwua, uhai mwovu.” Ndipo nikasema, “Una mguu hafifu.” Vema, hakuwa na dalili zake wakati huo. Lakini siku kadhaa baadaye, daktari alikuwa akimtibu mguu dhaifu.

Akasema, “Hiyo ni ya ajabu, Ndugu Branham.”

70 Sasa ninaenda kulazimika kusema mambo fulani hapa ambayo—ambayo yatakuwa ya kuwasha. Bali lazima ni—niseme ukweli, haijalishi ni kitu gani. Daima nimechukia kusema kwamba baba yangu alikuwa ni mwuza pombe haramu. Nilichukia kusema hilo, bali ni kweli. Naam. Kama kuna chochote kibaya, hebu—hebu—hebu tulinyoshe papa hapa, mchangoje mpaka tufike Huko juu. Nami ni—ninapenda kusema mambo mazuri, bali hatuna budi kuyasema mabaya, pia.

71 Mke wangu alikuwa chumbani, maskini, mwanamke mwenye nywele nyeusi. Ndipo Bibi Malicki akasema, “Hiyo ni ajabu, jinsi hiyo inavyofanya mkononi mwako.” Kasema, “Je! inafanya hivyo kwa mkono wa kila mtu?”

Nikasema, “La, mama.”

Kasema, “Waweza kueleza hilo?”

Nikasema, “La, mama.”

⁷² La, huwezi kueleza chochote cha Mungu. Huwezi kuzieleza kazi za Mungu. Huwezi kumfafanua Mungu. Mungu hafafanuliki. Kama angekuwa anaelezeka, isingetubidi kumwamini kwa imani.

⁷³ Nikasema, “Kazi za Mungu zimepita ufahamu. Unaona?” Nikasema, “Ni kazi ya Mungu, ambayo siwezi kueleza.”

Naye akasema, “Vema, mimi . . . Hakika hiyo ni ya ajabu.”

Ndipo, ndipo nikasema, “Vema, nitauweka mkono wangu. Naona hapo, hakuna kinachofanyika.”

⁷⁴ Nikasema, “Hakuna shida yoyote na mke wangu. Weka mkono wako, mpenzi.” Na punde tu mkono wake ulipougusa wangu, mke wangu mwenyewe, nikasema, “Una kivimbe kwenye ovari ya kushoto.”

Unakumbuka hilo, Ndugu Sharrit, chumbani usiku ule?

⁷⁵ Vema, miaka miwili baada ya hapo, maskini Sara wangu alizaliwa, miaka minne baada ya Becky. Nikamwambia daktari, hii . . . Wote inabidi wawe ni upasuaji, kwa sababu hawezi kuwazaa watoto kawaida; yeye alikuwa hivyo, familia yake iko hivyo. Ndipo nikamwambia daktari, “Angalia kwenye ovari ya kushoto, na wakati umemfungua, na uone kama hakuna kivimbe kwenye hiyo.”

⁷⁶ Akasema, “Ndugu Branham, sisi, nita—nitaangalia.” Lakini wakati ilininii . . . Wakati aliporudi, alisema, “Sikuona chochote, Ndugu Branham.”

Nikasema, “Sawa.”

⁷⁷ Miaka minne baadaye, maskini Joseph wangu akaja jukwaani. Nami ni—ningeushika mkono wake, kilikuwa kingalipo. Ndipo nikasema, “Daktari, iangalie ovari hiyo ya kushoto tena, utafanya hivyo?”

⁷⁸ Naye akasema, “Naam, Ndugu Branham.” Akaiangalia, nayo . . . “La, hakuna kitu hapo,” akasema.

⁷⁹ Nikaushika mkono wake. Nikasema, “Lakini kipo. Kipo. Hapa, inakithibitisha *hapa*.” Asingeweza kukipata.

Vema, ikaendelea, miaka ikapita.

⁸⁰ Mwaka jana, sisi, ulikuwa ni mwaka wetu wa ishirini na mbili tangu tuoane. Nami nilikuwa kwenye ziara ya kuwinda, kila fungate. Nami daima huenda mahali padogo huko juu kwenye kilele cha mlima, na ninakuwa na maombi kidogo huko juu, na kumtolea Mungu shukrani zangu kwa ajili ya mke mwema. Mke wangu amekuwa mpendwa kwangu, na kwa hiyo ninafanya hivyo kila mwaka.

⁸¹ Tulipokuja huku Arizona, kwa amri ya Bwana. Na mliona kwenye gazeti, nami nilikuwa na picha hiyo ndogo hapa, nilikuwa nikionyesha mtu fulani alasiri ya leo, jinsi jarida

lilivyoandika hilo. Ndipo nikasimama papa hapa kwenye mimbara hii, na kumwambia kila mtu hapa, “BWANA ASEMA HIVI, ‘Jambo fulani linakaribia kutukia. Niliona kundi la Malaika saba wakikutana nami, kaskazini mwa Tucson.’” Mnakumbuka hilo? Ni wangapi walikuwa hapa ndani niliposema hilo miaka iliyopita? Vema. Nanyi mnajua hasa jinsi ilivyotukia, vivyo hivyo.

⁸² Jarida hata lilichapisha picha, “Tumeona Nuru ya ajabu, maili ishirini na saba kwenda juu; maili thelathini kwenda juu, na maili ishirini na saba mlalo.” Unyevu huenda tu yapata maili nane au tisa kwenda juu, mwajua, nao hawawezi kuelewa kuwa Hiyo ilikuwa ni kitu gani. Sikusema neno juu yake, niliiacha tu ikapita; maana, haifaidi kitu, hata kidogo.

⁸³ Sawa tu na ilivyofanya kuhusu ile Nuru waliyoipiga picha, Malaika wa Bwana, wangali hawaamini Hiyo.

⁸⁴ Na sasa, kwa hiyo tunapokuja hapa nje, mimi daima kwenye mikutano, nikifanya kila niwezalo kwa Bwana. Lakini sifanyi yote yanipasayo kufanya, na—najua kwamba mimi hufanya makosa mengi sana.

⁸⁵ Na mke wangu imembidi awe yote mawili mama na baba, yote mawili, kwa hao watoto, maana niko safarini. Na uamuzi wake... Baba na mama wanapaswa kukubaliana juu ya maamuzi yao kwa ajili ya watoto wao. Bali mimi siko pale, niko katika utumishi wa Bwana. Na mke wangu sasa ana umri wa miaka arobaini na nne, mdogo tu kwangu kwa miaka kumi. Basi nilirudi kutoka kwenye mmoja wa mikutano, nami nilikuwa nimechoka. Ilikuwa kidogo zaidi ya (yapata) miaka miwili iliyopita, nadhani, tulipokuja huku. Nami nilikuwa nimekuwa nje, na nilikuwa nimechoka kwelikweli.

⁸⁶ Naye mvulana wangu mdogo, Joseph, yeye ni mvulana kabisa, na anakimbia huko shuleni ambako anasikia kila kitu. Siku moja nilipoingia, alisema jambo fulani, na kumwudhi mama yake. Ndipo—ndipo basi akanikimbilia. Sasa, mama yake alijua, yeye alijua angepata kichapo kutoka kwa mama yake.

Kwa hiyo yeye akaniambia, mama yake akaniambia, “Billy, mpe kichapo.”

⁸⁷ Naye akanikumbatia, kasema, “Baba, naomba radhi sana.” Alijua mahali pa udhaifu wangu.

Na kwa hiyo, “Loo,” nikasema, “mpenzi, tuachane nalo. Siwezi.”

⁸⁸ Na kwangu mimi na mke wangu, Biblia hii ikiwa mbele yangu, hatujakuwa na neno maishani mwetu. Bali mara moja, akiwa katika wakati huo wenye wasiwasi katika maisha, alipiga mlango moja kwa moja usoni pangu. Ndipo akasema, “Basi inakupasa kumtunza kwa muda,” akaupiga mlango, na kuingia ndani.

⁸⁹ Nikawaza, “Maskini jamaa mwenye mashaka! Jamani, ana hayo yote ya kupitia, mwenyewe.”

⁹⁰ Nikatoka nje, nami nikasema, “Joseph, njoo hapa,” nikasema. Nikamchukua. Nikasema, “Baba anafaa akupe kichapo. Unajua hilo. Bali,” nikasema, “kwa kuwa umetubu. Unaona? Bali, kumbuka, su—subira yangu inaenda kuisha, moja ya siku hizi. Na huko, huko kutubu, lazima uzae matunda yapasayo toba, na kunithibitishia kwamba kwa kweli unamaanisha. Unaona? Kama unanipenda, basi utanijali.”

⁹¹ Basi kwa hiyo nikatoka nje, nami nikasema, “Nitaosha kioo cha gari langu niondoe vumbi. Ndipo nikaanza kuosha kioo hicho.

⁹² Na, wakati nikiosha hicho, Sauti ikasema, “Rudi, ukamwambie asome Mambo Ya Nyakati 22.”

⁹³ Nikawazia, “Nimeninii tu—nimeninii tu—ninii. . .Sijui jinsi nilivyowaza hilo.” Nikawaza, “Vema, nimewaza tu hilo.” Nikaendelea kuosha.

⁹⁴ Ndipo ikaja tena, kubwa kwelikweli, “Nenda, kamwambie!” Vema, Hiyo ikanishtua.

⁹⁵ Nikaingia na kuisoma. Unajua ni nini? Ni wakati ambapo Miriamu alimdhihakiki Musa, kuhusu kumwoa msichana Mwethiopia. Ndipo Mungu akasema, “Ingekuwa afadhali baba yako akutemee mate usoni, kuliko kufanya hiyo.” Mnaona? Ndipo akawaita ndani, kasema, “Nenda, kamwite Miriamu, amepigwa kwa ukoma.” Kasema, “Nenda, kamwite Miriamu.” Ndipo Musa. . .Nayo Nguzo ya Moto ikashuka ikaja hekaluni. Naye Musa akasimama hapo. Na Mungu akazungumza nao. Akasema, “Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitajifunua Mwenyewe kwake. Nitanena naye katika maono, nizifunue ndoto, na kadhalika.” Akasema, “Bali mtumishi Wangu, Musa, hakuna aliye kama yeye nchini.” Akasema, “Hivi hamkumwogopa Mungu?” Naye Miriamu, akiwa ni nabii mke, akapigwa kwa ukoma. Ndipo Musa akamwombea, na akapona.

⁹⁶ Ndipo, hilo likanishtua. Nilikuwa nimesahau. Mimi, siku—sikutambua hilo, lakini Yeye alilitambua. Yeye Ndiye aliyelitambua hilo. Huyu alikuwa ni mke wangu, ningejitolea kufa wakati wowote kwa ajili yake. Lakini Mungu alilitambua. Sasa hii ni kweli, Biblia yangu ikiwa hapa mbele yangu.

⁹⁷ Ndipo nikaingia ndani. Naye alikuwa ameingia ndani chumbani na kufunga mlango, na alikuwa akishona kwenye cherehani. Ndipo nikabisha mlangoni, na nikasema, “Mpenzi, ninataka kuzungumza nawe kwa dakika moja.”

Akasema, “Unataka nini?”

⁹⁸ Nikasema, “Mpenzi, fungua mlango, moja kwa moja. Ninalo neno kutoka kwa Bwana.” Hiyo kwa namna fulani ilimtuliza kidogo, kwa hiyo akafungua mlango.

⁹⁹ Ndipo tukaingia. Na nikasema, “Mpenzi, sasa unajua, kadiri ninavyokupenda, si—si—sikuwazia chochote juu ya hilo.”

Akasema, “Vema, Bill, kama . . . nimevurugika akili sana!”

¹⁰⁰ Nikasema, “Ninajua. Lakini Yeye hakupendezwa na hilo. Hilo halikumfurahisha. Aliniambia moja kwa moja pale mtini, mti ule pale, maskini ule mti wa mtende mbele ya nyumba pale, nije hapa ndani na ‘kukusomea Andiko hili’” Ndipo nikasoma Hilo.

¹⁰¹ Basi anisaidie, katika siku chache, akawa na maumivu kwenye ubavu wa kushoto. Ilitubidi kwenda nyumbani. Nayo yakazidi kuwa mabaya. Nikamwombea. Yakazidi kuwa mabaya.

¹⁰² Nikampeleka kwa daktari rafiki yangu huko Louisville, Daktari Schoen, bingwa. Akamchunguza, kasema, “Bibi Branham, mwambie Ndugu Branham ninataka kumwona.”

Akasema, “Daktari, ulipata nini?”

Kasema, “Heri nimwambie yeye.”

¹⁰³ Kwa hiyo Meda akanipigia simu, nami nikaja. Naye akasema, “Ndugu Branham, ana kivimbe kwenye ovari yake ya kushoto, yapata ukubwa wa jozi.”

Ndipo nikarudi naye nyumbani, na nikasema, “Je! unakumbuka?”

¹⁰⁴ Akasema, “Hayo yalitendeka na Ndugu Sharrit, ikiwa sijakosea, huko California. Umeniambia hilo kwa miaka kumi na sita sasa.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli. Sasa ndiyo inaanza kuonekana.”

Akasema, “Bill, unafikiri ni kile nilichofanya asubuhi ile?”

¹⁰⁵ Nikasema, “Sijui, mpenzi, si—siwezi kusema.” Vema, tulikumbatiana na kuanza kulia, mbele za Bwana. Nikaingia chumbani na kumwombea, kwa moyo wangu wote.

¹⁰⁶ Daktari Schoen, nilimpigia simu tena, nikasema, “Daktari, tufanye nini?”

Akasema, “Kinapaswa kutolewa hapo.”

Nami nikasema, “Kiache tu kwa muda kidogo.”

¹⁰⁷ Akasema, “Nitakuambia, Ndugu Branham, labda ni heri nikutume kwa bingwa wa magonjwa ya wanawake, pamoja naye, rafiki mzuri. Yeye ni Mkristo, pia.”

¹⁰⁸ Nikasema, “Vema, vipi kuhusu wewe, Daktari?” Alitaka kuondoa hilo mikononi mwake, unaona.

¹⁰⁹ Akasema, “Nitakutuma huko juu.” Alinipenda, na aliiheshimu kazi yangu kwa Bwana. Basi alimwambia daktari huyu mwingine kuhusu hilo.

110 Nami nikampeleka huko juu. Nao wakakichunguza, na kuchora mchoro wake; wakachora mchoro na—na kile, ukubwa wake kilivyokuwa. Kasema, “Mrudishe katika yapata siku thelathini.”

111 Katika siku thelathini, nikakirudisha, nacho kikabadilika kutoka ukubwa wa jozi kikawa limau, haraka hivyo. Na miaka hiyo yote, kikawa hivyo.

112 Ndipo Bwana akanena nami, na kunituma tena, nikarudi huku nje.

113 Ndipo wakati tuliporudi kwenye likizo yetu nyingine, walipiga eksirei nyingine ya hicho, kilikuwa ukubwa wa chungwa. Akasema, “Bw. Branham, hakika ninathamini imani yako kwa Mungu Mwenyezi.” Akasema, “Mimi ni Mkristo, pia. Daktari Schoen huniambia kwamba wewe ni mponyaji wa imani.”

114 Nikasema, “Hakuelewa tu. Mimi si mponyaji wa imani.” Nikasema, “Ninamwamini tu Mungu.” Tena nikasema, “Tunaiielewa hali hii.”

Na yeye—yeye akasema, “Bw. Branham, unaye mke mwema.”

Nikasema, “Ninajua hilo vizuri sana!”

115 Kasema, “Hicho kikiwa chepesi, kitakuwa sugu, na ndipo hutakuwa na mke.”

Nami nikasema, “Ninatambua hilo, daktari.”

Kasema, “Hutaki kiondolewe?”

116 Nikasema, “La, bwana. Bali,” nikasema, “tunayo sababu. Kiache tu kiendelea kwa muda kidogo zaidi, sivyo?”

117 Na yeye akasema, “Vema, nitakuambia.” Kasema, “Wanasema unaishi Tucson sasa.” Naye aliniambia huyo bingwa, kasema, “Yeye ni rafiki yangu.” Kasema, “Nilihamia Tucson, na kujaribu kuishi huko, wakati mmoja.” Akasema, “Kulikuwa ni kukavu sana kwangu mimi.” Kasema, “Mtu huyu ndiye mzuri kuliko wote aliyepo, magharibi mwa Mississippi.” Kwa hiyo akasema, “Nitazituma eksirei na mchoro, na kila kitu, kwake.” Kwa hiyo, akazituma huko Tucson.

118 Naye mtu huyo, alipofika huku, siku thelathini zaidi, tulikitazama tena, mtu huyo alikitazama. Ndipo akasema, “Ni ukubwa wa tofaa, kinakuwa kikubwa kabisa. Hakina budi kutolewa, mara moja.”

119 Vema, ilinibidi kwenda. Nilienda huko kaskazini, na kwenda likizo yangu. Nikarudi, na kuenda New York, kwenye jiji la New York, katika Ukumbi Wa Morris, kwa ajili ya uamsho. Njiani nikirudi, ilinibidi kusimama Louisiana, huko kwa Ndugu Jack Moore.

¹²⁰ Nilimpigia mke wangu simu, usiku ukienda, naye akasema, “Mpenzi, kesho inanibidi kwenda kwa da—daktari tena, kwa ajili ya uchunguzi.” Naye anasema, “Bill, sijakuwa na uwezo wa kusogeza mguu wangu wa kushoto, juma hili. Unatokeza moja kwa moja kwenye gauni yangu.” Kimetokeza namna *hii*, kilikuwa kimevimba, kikikua haraka. Kisha kasema, “Ni chungu sana, hata siwezi kuinua mikono yangu.” Kasema, “Juma hili imenibidi tu kuinua mguu mmoja, wakati mmoja, na kutembea namna hiyo.”

¹²¹ Ndipo nikasema, “Mpenzi, atataka kukiondoa.” Kisha nikasema, “Kama akifanya hivyo, itakuwa ni kupitia wakati wa Krismasi; hatuwezi kurudi hapa, kurudi nyumbani.”

Naye akasema, “Ninajua hilo.” Akasema, “Vema, inatubidi kufanya nini?”

¹²² Nikasema, “Vema, mwambie tu, kama ‘angekiachilia tu kiendele mpaka baada ya Krismasi.’ Ndipo kitaondolewa, punde tu baada ya Krismasi. Maana, ninataka urudi nyumbani tena kabla ya kwenda hospitalini.”

¹²³ Na sasa alisema, “Sasa, ninaenda kesho, yapata saa tisa,” kitu kama hicho. Na hiyo ingekuwa tofauti kwa wakati wetu. Akasema, “Utakuwa na ibada yako ya kwanza basi huko Shreveport, halafu unipigie simu, baadaye.”

Nikasema, “Vema.”

¹²⁴ Mama mmoja aliye rafiki huko chini, mwanamke mzuri sana Mkristo. Walikuwa hapa Jumapili, sidhani kama wapo usiku wa leo. Watakuja. Norman, Bibi Norman. Huenda mko hapa, Bw. na Bibi Norman? Sijui kama wako hapa, au la, Ndugu na Dada Norman, kutoka Tucson. Yeye alikuwa ndiye... Nafikiri hawawezi kuja kila usiku, kwa hiyo atakuwa hapa kesho usiku, nadhani. Je! kuna ndugu, ndugu yake Dada Norman hapa? Nafikiri alikuja. Je! yupo hapa? Kuna... Familia, yeyote wa familia hiyo hapa, ninii ya Norm-...? Loo, naam, hakika. Wale pale, huko nyuma. Naam. Vema. Alimpeleka mke wangu huko.

¹²⁵ Sasa asubuhi ile niliyoondoka, nyumbani kwetu, ilitubidi daima kuamka, na wakati tukienda kuomba; tukiondoka, tungechukua watoto na sisi sote, tunasimama tumezunguka na kuelekea picha ya Yesu, sebuleni mwetu, *Kichwa cha Kristo katika Umri wa Miaka Thelathini na tatu* iliyochorwa na Hoffman. Nasi sote tungekusanyika pale, watoto, na kila mmoja wao angeniombea. Mke angeniombea, na kisha ninamwombea. Ndipo ningeenda ng’ambo, popote pale. Halafu tunajikabidhi kwa Bwana, kwa ajili ya huduma Yake.

¹²⁶ Mnajua, nilipoteza mke wangu, wakati mmoja, nilipokuwa mvulana, mama yake Billy. Nami nilikuwa pale nyumbani kwa siku mbili ama tatu, na, mnajua, watoto na kila mtu pale, na kila mtu ameondoka wakati huo. Ulikuwa ni upweke. Ukarejesha kumbukumbu hizo zote.

¹²⁷ Basi asubuhi hiyo, mapema, niliamka, Billy na Loyce pale walikuwa wakiningojewa. Ndipo nikapiga magoti, na kuivuta maskini stuli hii ya kale, yenye matakia. Nikapiga magoti, nikaangalia juu, na kusema, “Loo, jinsi ninavyowakosa!” Nikasema, “Baba wa Mbinguni, niko njiani sasa kuelekea Shreveport. Ninaomba kwamba utanisaidia huko. Na kunibariki, unipe nafsi, Bwana, kwa ajili ya Ufalme Wako. Nitumie vyovyote upendavyo. Niko mikononi Mwako.” Nikasema, “Mbali huko kupita majangwa, yuko maskini mke wangu mwaminifu, akisubiri asubuhi ya leo. Yeye anaenda huko juu, ili kujiandaa kwa ajili ya huo upasuaji.” Nikasema, “Bwana, nilimwambia, jana usiku, ‘Mwombe daktari auahirishe mpaka baada ya Krismasi.’ Je! nilikosea? Je! huenda hicho kikawa sugu? Kama nilifanya hivyo, na kumwambia amwombe huyo daktari, ‘kuahiririsha,’ na, kati ya wakati huo, kingekuwa sugu na nimpoteze, nisingejisamehe kwa hilo.”

¹²⁸ Nikasema, “Bwana, nimezungumza na Wewe sasa kwa miaka hii miwili, naam, miaka kumi na sita, bali,” nikasema, “miaka miwili iliyopita tangu jambo hilo kutendeka.” Nikasema, “Baba, hajawahi kosa kuwa mke halisi kwangu. Ninapokuwa tayari kwenda kwenye huduma, hakuna hata wakati mmoja aliowahi kunung’unika, si hata wakati mmoja. Daima anazifua nguo zangu, na kufua mashati yangu, na kadhalika, na kuzitayarisha zote kwa ajili yangu. Na halafu ninapokuja nyumbani, nimechoka sana, siwezi... Na ni, kwa kawaida, mwanamke angetaka mume wake awe pamoja naye. Nami ninaingia, watu wakiingia kwa wingi, ninafanya nini? Ninaondoka kwenda kwenye ziara ya kuwinda au ziara ya kuvua samaki. Je! aliwahi kunung’unika? Si hata wakati mmoja. Nenda ukatayarisha nguo zangu, na uniache niende, ‘Hiyo ni sawa.’ Maskini jamaa mdogo, mwenye umri wa miaka arobaini na nne, mwenye kichwa cheupe kama theluji, akisimama kati yangu na umma.” Nikasema, “Mungu, hakumaanisha hilo, asubuhi ile. Kwa kweli hakulimaanisha, Baba. Matendo yake yanaonyesha kwamba hakulimaanisha. Alikuwa tu na mvurugiko wa akili.”

¹²⁹ Basi nisaidie, kwa mara ya tano ambayo limetendeka! Tangu wale kuchakulo; na halafu huko chini Kentucky; halafu watoto wa Wright huko chini; halafu kile kimbunga mlimani, ambacho sina wakati kuwaelezeni usiku wa leo; na wakati huu, hakika tu kabisa! Kukaja ile Nuru, ikining’inia pale, na Hiyo ikasema, “Simama kwa miguu yako.” Nami nikasimama. Akasema, “Lolote ukakalosema, hivyo ndivyo itakavyokuwa.”

¹³⁰ Nikasema, “Mkono wa Mungu utakiyeyusha hicho kivimbe kabla ya mkono wa daktari kukigusa.”

¹³¹ Nitakuwa na Bibi Norman hapa kesho usiku. Sikumpigia simu, ilikuwa moja kwa moja... Billy na Loyce walikuwa wakiningojewa. Tukaenda Shreveport, nikaenda kwenye simu ili kumpigia tulipofika huko.

¹³² Alikuwa ameenda kwa daktari. Naye Bibi Norman ilibidi amsaidie huko, pamoja na nesi, chumbani, kuvaa gauni yake, ili kuja kwenye meza. Ndipo wakaziweka mashine, pamoja na michoro na eksirei, na kadhalika. Akasema, “Umekuwa ukijisikia namna gani, Bibi Branham?” Akasema, . . .

¹³³ Ndipo, daktari, tukafungua barua, kuona alichandika ndani yake, kwa daktari huyu. Kasema, “Bibi Branham ni mwanamke mzuri sana, na mume wake ni mtu mzuri. Yeye ni mponyaji wa imani, bali hakatai wewe kufanya upasuaji. Daktari, kinafaa kiondoke mara moja!” Hiyo ni kusema, tulikuwa tumesoma hiyo, unaona, “Hicho kivimbe kinafaa kiondolewe mara moja, la sivyo Bibi Branham atakufa.”

¹³⁴ Ndipo basi mara daktari alipojitokeza, kuinua shuka, kugusa ubavu wake, kitu Fulani baridi sana kilipitia juu yake, nacho kivimbe kikaondoka. Hakuna kivimbe. Naye daktari. . . alilala pale, naye akagusa, akasema, “Bibi Branham, hicho kivimbe kilikuwa upande wa kushoto, sivyo?”

Akasema, “Ndiyo, bwana, kilikuwa.”

¹³⁵ Kwa hiyo akageuza mgongo wake kwenye mashine ya eksirei, akaenda akaleta michoro yake, akapitia uchunguzi tena. Akasema, “Bibi Branham, siwezi kueleza, lakini kivimbe hicho hakipo tena. Hicho kivimbe kimetoweka.”

¹³⁶ Sasa, hiyo ni kweli, kwa hiyo nisaidie! Mungu Mwenyezi anajua kwamba ni kweli, nikisimama hapa. Mnaona, kama tu ilivyosemwa! Bali “mkono wa daktari,” yeye alisema, “haukuwa mbali *sana*” naye, mpaka kitu Fulani baridi kikapitia juu yake. Ilikuwa vigumu kwake. . . Ilibidi asaidiwe na Bibi Norman na hao, (na jamaa hao kule nyuma wanaweza kukuambia kuhusu hilo), akasaidiwa kupanda juu mezani. Nayo michoro na eksirei, na kila kitu pale, cha kivimbe. Na hapakuwapo hata dalili yake moja. Wala hajawa na dalili yoyote tangu wakati huo. Na hiyo ilikuwa yapata majuma mawili kabla ya Krismasi.

¹³⁷ Mungu angali ni mwaminifu kwa Neno Lake! “Mbingu na nchi zote zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe.” Mungu, Yule awezaye kuumba kuchakulo, Yule awezaye kuondoa vivimbe, Yeye angali ni Mungu yeye yule usiku wa leo, kwa kuwa ni Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Baba wa Mbinguni, ambaye ni shahidi wangu, nikiwa na Biblia hii juu ya moyo wangu, anajua kwamba kila neno la hiyo ni kweli kama ni juavyo kusema. Ingenifaidi nini kusema jambo lisilo kweli, enyi marafiki? Ninasema haya kwa kusudi gani? Kwamba yaweze kuwatia moyo kuamini.

¹³⁸ Sasa, karama hiyo kuu! Mingine nimejaribu kueleza na kusema jinsi ilivyofanywa. Huu hauwezi kuelezewa. Ngojeni tu. Hautakuwa kazini kikamilifu sasa. Ngojeni mpaka lile Baraza la Mekanisa litakapoleta yale mateso, hapo ndipo litakapotukia.

Hiyo ndiyo sababu nimerudi miongoni mwenu, kuwaombea wagonjwa. Sijawa ila na kitu kimoja ambacho Yeye aliniambia katika maisha yangu ambacho ninajua hakijatendeka bado, kwamba namna fulani ya jengo au hema mahali ambapo patakuwa na chumba kidogo na itanibidi kuingia ndani ya hicho kuwaombea wagonjwa. Hicho hakijatendeka bado kama nijuavyo mimi. Hicho ndicho kitu pekee nijuacho.

¹³⁹ Na wakati Yeye anaposema Maneno hayo, kulisema, Baba wa Mbinguni anajua kwamba ninasimama hapa usiku wa leo na Yeye angeweza kuniua papa hapa katika mimbara hii. Naam, bwana, hakika Yeye angefanya hivyo; nami ninajua hilo, ninajua hilo vizuri sana. Nami ninajua kuna hadithi nyingi sana leo hii, ambazo, si—siwajibiki kwazo. Ninawajibikia tu yale ninayosema. Mimi, inanibidi kuwajibikia yale ninayosema. Na hiyo ni Kweli. Naye Baba wa Mbinguni anajua kwamba hiyo ni kweli.

¹⁴⁰ Sasa utaamini Yesu Kristo Mwana wa Mungu alikufa kwa ajili ya dhambi zako, na alijeruhiwa kwa makosa yako, kwa mapigo Yake wewe uliponywa? Mnaamni hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Katika siku hii, wakati inapoonekana tu kana kwamba kila kitu ni giza, na cheusi na chenye ukungu, lakini hata hivyo Yesu anabaki yeye yule! Hivi hamwamini hilo? [“Amina.”] Yeye yupo hapa usiku wa leo!

¹⁴¹ Ninataka mtu fulani asimame na kuniambia chochote nilichowahi kusema katika Jina la Bwana, kando na hicho, ila kilichotukia. Na ni mara mia ngapi ambapo mmemwona Yeye akilisema, Hilo kamwe halijawahi kushindwa! Ni kitu gani ninachojaribu kuwaambieni? Haiwezekani kabisa kwa mwanadamu kufanya hilo. Ni Yesu Kristo miongoni mwa watu. Ni Kristo miongoni mwetu.

¹⁴² Leo hii, wakati madhehebu yanasema, “Njoo *hapa*, na njoo *pale*,” ni ule mtindo wa kale wa shule fulani ama kitu kingine; ambacho ni sawa kabisa, inabidi kiwepo, ni sehemu ya mdundo.

¹⁴³ Bali, kwangu mimi, Yeye yu hai usiku wa leo, akiwa tu na mamlaka na nguvu, kulifanya kila Neno halisi, alivyofanya kule nyuma.

Hebu na tuombe.

¹⁴⁴ Bwana Yesu, Wewe ulisema, “Mbingu na nchi zitapita, Maneno Yangu hayatapita.” Hivyo ndivyo wanafunzi walivyojua kwamba Wewe ulikuwa ni Yule uliyekuwa, kwa sababu ulitambua mawazo yaliyokuwapo moyoni. Biblia ilisema, katika Waebrania 4, kwamba, “Neno la Mungu ni kali, lina nguvu zaidi kuliko upanga ukatao kuwili, hata ni Tambuzi la mawazo na makusudi ya moyo.” Neno la Mungu katika manabii, lilifanya jambo lilo hilo. Katika wenye hekima waliokwisha ondoka, lilifanya jambo lilo hilo. Ndani ya Bwana Yesu Kristo, lilifanya jambo lilo hilo. Baba, Mungu, acha Neno Lako linene, usiku wa

leo, kusudi wagonjwa waweze kuona kwamba Wewe una haja na kuponywa kwao, na umeshawaponya, Baba, na uwajalie kuwa na imani ya kuamini. Katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁴⁵ Sasa wakati mpiga piano na mpiga kinanda, mkiweza, kwa utulivu, kwa utulivu sana, “Amini Tu.”

¹⁴⁶ Na, Billy, nilisahau kukuuliza, ni namba zipi ulizosambaza? [Ndugu Billy anasema, “A, moja hadi mia moja.”—Mh.]

A, moja hadi mia moja. Hebu na tuanze kusimama.

¹⁴⁷ A, namba moja hadi namba tano, simameni kama mnaweza. Kama huwezi, inua tu mkono wako. Namba moja hadi namba tano. Moja, mbili, tatu, nne, nadhani ndiyo hiyo, njoo papa hapa. Moja, mbili, tatu, nne, tano, A. Wakati wanapokuja, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, simama kama unaweza. Sita, saba, nane, tisa, kumi, naomba msimame. Kadi za maombi, sita, saba, nane, tisa, kumi. Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Vema, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Njoo moja kwa moja huku, endeleeni tu kuja. Hiyo ni kweli. Vema, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini.

¹⁴⁸ Sasa, mvulana huyo anakuja, baadhi yao, huzisambaza kadi, na kuzichanganya, hatujui namba ziko wapi, au chochote. Mnamwona akifanya hivyo, nyinyi wenyewe, kuchanganya kadi. Anakupa ile kadi unayotaka, na—na hivyo mnaitwa tu kwa kadi.

¹⁴⁹ Si lazima uwe na kadi. Amini tu, popote ulipo. Umekuwa kwenye mikutano, unajua, unajua hayo yote yanahusu nini. Vema.

¹⁵⁰ Nilikuwa wapi, nilipoachia, ishirini? [Mtu fulani anasema, “Ishirini.”—Mh.] Ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, ishirini na tatu, ishirini na nne, ishirini na tano. Vema.

¹⁵¹ Ni wangapi walio wagonjwa na hawana kadi ya maombi, hebu tuone mikono yenu. Vema. Popote katika jengo pale, vema, aminini tu sasa.

¹⁵² Sasa tunajaribu kusema nini, ni nini tunachotaribu kuwakilisha? Yesu Kristo. Ni wangapi wanaelewa hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wanajua ya kwamba katika siku ya kuzuriwa na Yeye, duniani, kwamba Yeye alikuwa ni Mungu aliyedhihirishwa katika—katika mwili uitwao Yesu, huyo alikuwa ni Mungu ndani ya Mtu? Hiyo ni kweli. Sio tu nabii; Yeye alikuwa ni Mungu! Na Yeye. . . Manabii walikuwa na sehemu yao ya Neno, *sehemu* yao ya Neno, sehemu waliyopewa kwa ajili ya wakati huo. Lakini Yeye alikuwa ni utimilifu wa Neno! Ni wangapi wanajua hilo? [“Amina.”] Yeye alikuwa ni Neno Lenyewe. Sasa kuna sehemu iliyotengwa ya Neno kwa ajili ya siku hii. Je! hiyo ni kweli? [“Amina.”] Huyo angekuwa ni Yeye tena. Je! hiyo ni kweli? [“Amina.”] Kwa hiyo hiyo inamfanya Yeye kuwa ni yule yule jana, leo!

153 Tuna wangapi? [Mtu fulani anasema, “Ishirini na watano.”—Mh.] Ishirini na watano, hebu tuchukue tu hao. Sasa, tukienda mbali zaidi ya hapo, nanyi mnataka, kuna wakati wowote uliosalia; nina kama dakika ishirini, au kitu kama hicho. Tunaleta. . . Sasa kumbukeni, kama kuna watu hapa ndani walio na kadi za maombi, ishikilie hiyo kadi ya maombi. Tunaenda kumwomba kila mtu atakayekuja, atakayekuja na kupata kadi ya maombi, ikiwa tu utakaa nasi. Ikinibidi kukimbia, mchana na usiku, nitawafikia. Kwa msaada wa Bwana, hakika nitawafikia.

154 Sasa ikiwa mtanisikiza tu kwa makini! Sasa ni wangapi hapa ndani, wanaoketi hapo nje, wanaoamini kwamba una imani ya kutosha kumgusa Yeye? Hilo ni jema sana. Naam. Sasa hebu tusiache iwe ni bure, enyi marafiki.

155 Sasa yupo mama aliyeketi *hapa* kwenye kiti cha magurudumu, na yupo mwanamume aliyeketi *pale* kwenye kiti cha magurudumu. Ninaweza kuona kwamba ni wagonjwa. Bila shaka, wao si wagonjwa, labda, bali wanateseka. Msife moyo, dada na ndugu. Mnajua, kama ningeweza, kama ningeweza kuwaponya, mnajua ningekuja nifanye hivyo, sivyo? Hakika ningekuja. Kama nisingefanya hivyo, sina ninii—sina shughuli kusimama nyuma hapa. Kama nina ukatili moyoni mwangu; kwamba ningekuondoa kwenye *hicho* kiti cha magurudumu, na wewe kutoka kwenye *hicho* kiti cha magurudumu, na nisifanye hivyo, ningekuwa ni mtu katili.

156 “Vema,” mnasema, “kwa karama ya Mungu, unapaswa kufanya hivyo, kwa vyovyote vile.” Ngoja kidogo. La, hivyo ndivyo hamsomi Maandiko ipasavyo.

157 Yesu alipitia mahali palipokuwa na maelfu ya viwete, walemavu, vipofu, viwete, na waliopooza, wala hakuwagusa. Ndipo akamwendea mtu ambaye alikuwa labda na ugonjwa wa tezi dume, au kitu kingine. Alikuwa amedumaa, alikuwa nao kwa miaka thelathini na mitano. Angeweza kutembea. Angeweza. . . miaka thelathini na minane, naamini ilikuwa. Mnaona, kuna baadhi yenu. . .

158 Hakika, vipi kama huyo alikuwa ni mke wangu ameketi *hapo*, au mama yangu, mke wangu, binti yangu; mnaona, ama ndugu yangu, baba yangu ameketi *hapo*? Loo, kama lolote lingeweza kufanywa, hakika ningetaka lifanywe. Mnaona?

159 Lakini, mnajua, huenda kuna mtu ameketi moja kwa moja *hapa*, anaonekana mwenye afya kabisa, yu karibu zaidi na kifo kuliko *hao* walivyo; akiwa na tatizo la moyo au kansa, mnaona, karibu zaidi na kifo. Lakini je! ni vigumu zaidi kwa Mungu kuiponya kansa, au kilema? Hakuna tofauti. Yeye anahitaji tu, “Ukiamini.”

160 Sasa, kwa ajili yangu, kuwaonyesha kwamba isingeweza kuwa ni mimi, ningekuja niifanye sasa hivi. Kama ningeweza kuifanya, ningefanya maonyesho kutokana nayo, nadhani.

Ningesema, “Hebu nimlete huyu mwanamume na mwanamke hapa juu mimbarani, niwaonyeshe jinsi nilivyo mtumishi mashuhuri wa Kristo.” Ningetamka maneno fulani juu yake, “Amka sasa na uondoke ukitembea!” Mnaona, ningefurahia kufanya hivyo. Umati wote ungepiga tu mayowe, na kusema, “Mungu asifiwe! Mtumishi wa Mungu mashuhuri na mwenye nguvu jinsi gani, ndiye Ndugu Branham!” Mnaona? Hapana, hiyo, hiyo ingekuwa ni kosa, mnaona.

Bali sasa Yesu anaweza kuwaponya wote wawili, usiku wa leo.

¹⁶¹ Lakini, mnaona, mtu akilemaa tu kidogo, wanaanza, moja kwa moja wanashuka, (hawataki kuwazia hilo), lakini huko chini, wanaanza kuwazia, “Mimi nimepita kwenda, unaona. Mimi—mimi siwezi.” Usifanye hivyo. Usifanye hivyo. Mnaona, wewe amini. Na kama ningeweza, ningeninii. . . Lakini, sasa, kama utaondoa tu hayo mashaka yote kutoka moyoni mwako, kabisa usiruhusu chochote kuingia kitakachozuia.

¹⁶² [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Umejikunyata na unateseka, tangu kuzaliwa; jinyooshe tu, na uondoke ukitembea, mzima na mwenye afya. Unaona? Hayo ni matamshi, madaktari na Mayo Brothers. Nanyi mliona hilo katika *Reader's Digest*, si muda mrefu uliopita, Donny Morton, *Mwujiza wa Donny Morton*. Yule mtoto mchanga kule California, kwenye Assemblies of God, kule chini kwenye ile shule, Southwestern Bible School, mtoto yule alipindika sana na kuteseka hata John Hopkins na Mayo Brothers wakasema, “Hamna nafasi duniani kwa ajili yake.” Bali Bwana ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ilikuwa tofauti, mnaona.

Usiende, bila tumaini.

¹⁶³ Sasa, sasa kwa dakika chache zijazo, tunaenda kuomba sasa. Imefikia yapata dakika kumi na mbili, labda tunaweza kumaliza mstari wa maombi. Na sasa nikimaliza hao, labda, na niwe na wakati mwingine zaidi. . . Niliahidi kuwaacha saa tatu u nusu. Nyinyi angalieni hiyo. Vema. Ndipo tutaninii, kile tutakachokosa usiku wa leo, tutachukua kesho usiku.

¹⁶⁴ Sasa kila mtu atakuwa akiomba. Na nyinyi nyote huko nje ambao sasa, ambao ni, hawana kadi za maombi, au walio na kadi za maombi, chochote kile, nyinyi anzeni tu kuomba. Mnaona, imani yako itafanya kile hasa Yesu alichofanya katika siku zilizopita. Unaweza kugusa vazi Lake. Sasa iwapo kila mtu atakuwa na kicho kabisa, msisogee huku na huku. Iweni na kicho kabisa, kwa kitambo kidogo tu.

¹⁶⁵ Njoo, bwana. Hatufahamiani, nadhani. Kama ningaliweza kukusaidia, ningalikusaidia. Wewe, wewe unajua hilo. Ni—ningefurahia kufanya hivyo, bali siwezi. Kwa kweli, ni mtu mwingine unayesimama kwa ajili yake, anayetaka kuombewa. [Mtu huyo anasema, “Naam, bwana.”—Mh.] Unaamini Mungu

anaweza kumponya? [“Naam, bwana.”] Hawapo wakati huu. [“La, bwana.”] Wako mbali na hapa. [“Naam, bwana.”] Ni ugonjwa wa kansa. [“Naam, bwana.”] Je! hiyo ni kweli? [“Naam, bwana.”] Je! unaamini kwamba wataponywa? [“Naam, bwana. Ninaamini.”] Nenda, na itafanyika, kama ukiamini. Hayo tu ndiyo yakupasayo kufanya. Hiyo si ni ya ajabu? Mungu akubariki.

¹⁶⁶ U hali gani? Vivyo hivyo hatufahamiani. Mwanamume tu aliyeingia humu. Sikujui, sijawahi kukuona. Bali, na wewe upo hapa. . . *Hii*, hii Biblia ya thamani, inashikilia ahadi; hiyo ni kusema, Hiyo ni Neno la Mungu. [Mtu huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Nayo Biblia inasema, Humo ndani, kwamba, “Neno la Mungu huyatambua mawazo, shauku na makusudi ya moyo, na kadhalika, hunena Neno hili lililoandikwa, pia hulithibitisha kuwa ni kweli, kwa kutabiri, na Mungu kufanya Hilo kuwa halisi.” [“Amina.”] Kama Yeye alivyosema, “Iwe nuru, na kukawa nuru.” [“Hiyo ni kweli.”] Ninasema tu hilo, kuzungumza nawe, kama vile Bwana wetu alivyozungumza na yule mwanamke kisimani, kama alivyomwona Simoni, na kadhalika.

¹⁶⁷ Umekuwa na shida fulani. Ufefanyiwa upasuaji. Pamepasuka tena. [Mtu huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Unaelewa ninapomaanisha, na ni kwa nini siwezi kulisema moja kwa moja hapa. [“Naam, bwana. Hiyo ni kweli.”] Nawe unaelewa ni kwa nini. Hiyo si ni kweli? [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli. Siwezi kulisema hapa, lakini wewe unajua. Nilikuhisi pale pale ulipowazia, “Sijui kama atasema hilo, ama kama,” namna hiyo. [“Hiyo ni kweli.”] La, sitalisema, kwa sababu siwezi kulisema hapa. Bali itakuwa sawa sasa. [“Asante, Yesu.”] Nenda, amini. Mwamini Mungu.

¹⁶⁸ U hali gani, mama? Je! unamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu? Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? [Mwanamke huyo anasema, “Hakika ninaamini!”—Mh.] Ninathamini hilo. Kama kuna njia yoyote ya kukusaidia, nitakusaidia. Ipo njia moja tu niwezayo kukusaidia, hiyo ni kwa yale niyaonayo. Ninaweza tu. . . Yale nionayo, basi ninayasema. Ikiwa siwezi kuyaona, vema, basi mimi. . . siwezi kuyasema, bila shaka, mpaka niyaone, maana hayana budi kutoka Kwake. Ni ninii ya Kiungu. . . Ni karama ya Kiungu ya Mungu, inayotoka kwa Mungu.

¹⁶⁹ Tatizo lako liko kwenye jicho lako. Una donda ndugu katika jicho lako. Huwezi kuliona, bali liko kwenye jicho lako la kushoto. [Mwanamke huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ili uweze kujua hili sasa, kwa kuwa mtu fulani huko nje anaweza kulisema. Ninaona anayo matatizo mengine zaidi. Anayo matatizo na titi lake la kushoto, pia. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli, sivyo? [“Hiyo ni kweli.”] Sasa unajua. Hapa, kama hilo lingekutatiza, hebu nikwambie. Hutoki hapa. Unatoka

mbali na hapa. Unatoka Louisiana. [“Hiyo ni kweli.”] Rudi, na umwamini Mungu, nawe waweza kuponywa hilo. Amina. Amini, kwa moyo wako wote. Mwamini Mungu. Usitie shaka. Amini tu.

U hali gani? Umesongwa kwelikweli.

¹⁷⁰ Huyu mtu anasumbuliwa papo hapo na ukandamizaji, pia; kidogo ana mvi, amevaa suti ya kijivu, ameketi, akiniangalia mimi. Una hali ya kukandamizwa, sivyo, bwana? Imekuacha sasa. Imekwisha. Sifa kwa Mungu!

Aligusa kitu gani? Si mimi.

¹⁷¹ Hiyo hata ilimpa mwanamume yule, nyuma yake, ujasiri fulani. Hujataka kuamini kwamba una TB, matatizo. Unamkubali Yesu sasa kama Mponyaji wako? Vema, unaweza kupata uponyaji wako. Amina. Amini kwa moyo wako wote. Amina. Hiyo ndiyo njia ya kuifanya. Loo, jinsi ilivyo ya ajabu!

¹⁷² Mnaamini, nyinyi nyote? Wanaume usiku wa leo, inakuja moja kwa moja kwenye safu ya wanaume!

¹⁷³ Mwanamume huyo anayeketi moja kwa moja nyuma yake pale, anashangaa kabisa kuhusu hayo. Una baridi yabisi. Unaamini kwamba Mungu ataiponya? Unaamini? Basi unaweza kuupokea! Loo, jamani!

¹⁷⁴ Enyi wanawake, nyinyi...Iko moja kwa moja kwa wanaume, inaonekana, inaenda tu na wanaume usiku wa leo. Ajabu! Shukrani kwa Mungu!

¹⁷⁵ Huyu hapa mwanamume mwingine, anayeketi moja kwa moja hapa, ana ngiri maradufu. Je! unaamini kwamba Mungu ataiponya hiyo ngiri? Amina. Unaweza kuupokea.

¹⁷⁶ Huyu mwanamume mwingine, wa pili nyuma yake, ana ngiri, pia. Unaamini, bwana? Unaweza kuupokea, pia, ikiwa tu utaamini. Amina. Haleluya!

¹⁷⁷ Je! unamwamini Mungu? Kuwa tu na imani. Usitie shaka. Hakuna umbali, kwa Mungu. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁷⁸ Huyu hapa mwanamume aliyeketi moja kwa moja kupitia hapa. Ninamnyoshea kidole changu moja kwa moja. Amevaa miwani, mwenye mvi. Ana kisukari. Kama ataamini kwa moyo wake wote, Mungu atamponya. Mke wake ameketi moja kwa moja karibu naye pale. Naam, weka mkono wako juu yake, ana shida ya utumbo mpana. Weka mkono wako juu yake, na uamini kwa moyo wako wote, nanyi nyote wawili mnaweza kuponywa.

Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁷⁹ Shida yako ni kuganda kwa damu. Ni kwenye mkono wako wa kushoto. [Mwanamke huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ulikuwa na kansa. [“Hiyo ni kweli.”] Ulifanyiwa upasuaji. [“Ndiyo.”] Walikupa tiba fulani. [“Ndiyo.”] Tiba hiyo ilisababisha huku kuganda kwa damu kuingia hapa,

katika hali mbaya. Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya? ["Ninaamini."] Basi jinsi ulivyoamini, hivyo na ifanyike kwako. Katika Jina la Bwana Yesu, jalia aponywe.

¹⁸⁰ Unaonekana kama mwanamke mwenye afya, mwenye nguvu. Je! unaamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, anaishi? [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo, ninaamini."—Mh.] Je! unaamini kwamba Yeye yupo hapa usiku wa leo? ["Ndiyo, ninaamini."] Kama ningeweza kukuambia jambo lililo shida yako, hivi ungemwamini kwa moyo wako wote? ["Ndiyo."] Umepangiwa kufanyiwa upasuaji. ["Ndiyo."] Ni tatizo la kike. ["Ndiyo."] Shida ya kina mama. ["Ndiyo."] Inakubidi kufanyiwa upasuaji. ["Ndiyo."] Unaye mtu fulani pamoja nawe, ambaye anahitaji kabisa kufanyiwa upasuaji, pia, mtu mwenye umri mdogo zaidi yako. ["Ndiyo."] Hiyo ni kweli. ["Ndiyo."] Hiyo ni kweli kabisa. Halafu, una mtu fulani unayemwombea, huyo ni mume wako. ["Ndiyo."] Hajaokoka. ["Loo, ndiyo!"] Naye hayupo hapa. Wewe amini kwa moyo wako wote, naye ataokoka, nawe haitakubidi kufanyiwa upasuaji. ["Loo!"] Nenda sasa na uamini, kwa moyo wako wote. Amina. Amina.

Kuwa na imani katika Mungu!

¹⁸¹ Ninaweza kuona jinsi unavyotembea. Mungu pekee huponya kansa. Lakini Mungu anajua jinsi ya kufanya hivyo. Je! unaamini kwamba atakufanyia hivyo? [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo. Ndiyo."—Mh.] Basi ninaweka mikono yangu juu yako, dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji wako. Amina. Nenda sasa, usitie shaka, amini kwa moyo wako wote.

¹⁸² Njoo, dada. Ugonjwa wa pumu, tatizo la kike. Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya? [Mwanamke huyo anasema, "Ninaamini."—Mh.] Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina. Vema.

¹⁸³ Unaugua kisukari. Je! unaamini kwamba Mungu atakupua afya, akutibu na kufanya... na kukuponya? [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo. Ninaamini."—Mh.] Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe. Sasa kama unamwamini Mungu, ukiwekewa mikono namna hiyo, itatendeka.

¹⁸⁴ Naam, bwana, tatizo la mgongo na tatizo la tumbo. Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya? [Mwanamume huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Basi nenda, katika Jina la Yesu Kristo, ukaponywe, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

Kila mtu anaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

¹⁸⁵ U hali gani, bwana? Hakika, unaona una tatizo la tezi, nalo limekufanya kuwa na tatizo la moyo. Je! unaamini kwamba Mungu ataponya moyo wako na kukupa afya? [Mtu huyo anasema, "Amina."—Mh.] Nenda, katika Jina la Yesu Kristo, na uponywe.

¹⁸⁶ Ninataka kuwaonyesha kitu. Nitaivua saa hii, kuivua. Je! unaamini Mungu anaweza kuponya tatizo la pafu, na kukufanya mzima? [Mwanamke huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Vema, hakika Yeye anaweza. Je! uliona vile hilo lilitendeka? Vema, Bwana akubariki, nenda ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁸⁷ Sasa hebu nishike mkono wako. Ninataka uangalie mkono wangu, wa kawaida kama mkono wa watu wengi. Je! hiyo ni kweli? Niliweka mkono wangu juu yake, sasa umebadilika, unavimba, vivimbe vidogo vidogo vikitokea juu yake. Una tumbo lenye vidonda. Je! unaamini kwamba Mungu ataliponya? Je! unaupokea uponyaji wako sasa? [Mwanamume huyo anasema, “Ninaamini.”—Mh.]

¹⁸⁸ Bwana Mungu, katika Jina la Yesu Kristo, mponye mtu huyu. Kwa wakati huu, Bwana, mwondolee huo, ili aweze kuona na kujua kwamba ni kweli. Mimi... Imelandikwa katika Biblia, “Katika Jina Langu watatoa pepo; hao waaminio.” Bwana, ninaamini. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia ibilisi huyu amwondokee ndugu yangu. Amina.

¹⁸⁹ Hebu tuone mkono wako tena. Sasa hauonekani kama ulikuwa nao, sivyo? [Mtu huyo anasema, “La, hauonekani.”—Mh.] Umeponywa. Nenda, uwe mzima!

¹⁹⁰ Ugonjwa wa pumu. Unaamini Mungu atauponya? [Mtu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Nenda ukapumue, katika Jina la Bwana Yesu Kristo, ukapate afya. Amina. Kuwa na imani.

¹⁹¹ Mungu huponya tatizo la mgongo, na kuwafanya watu wazima. Je! unaamini hilo? [Mtu huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Vema, nenda zako, na useme, “Asante, Bwana Yesu. Nami nitaponywa!” [“Haleluya!”] Usitie shaka hata kidogo; kwa moyo wako wote. Amina.

¹⁹² Vipi kama nilikuambia uliponywa kwenye kiti, je! ungeamini? [Mtu huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Vema, nenda zako tu, ukishangilia, ukisema, “Asante, Bwana Yesu,” nawe utapata kile ulichoomba. Vema.

¹⁹³ Njoo, bwana. Je! unaamini? [Mtu huyo anasema, “Naam, ninaamini.”—Mh.] Ninataka kukuonyesha, ili ione kane mikononi mwako. Niambie... Angalia mkono wangu hapa, hauna kasoro yoyote. Unaona hapa ndani? [“Hamna kitu.”] Sasa unabadilika, ulivimba, vitu vidogovidogo vyeupe vinapitia juu yake. [“Naam.”] Je! ungependa kula chakula chako cha jioni, na kujisikia vizuri tena? [“Naam.”] Je! unaamini unaweza? [“Naam.”] Je! unaamini mambo haya unayoona yanatoka kwa Mungu? [“Naam, hakika ninaamini.”] Sasa angalia moja kwa moja kwenye mkono wako tena... mkono wangu tena, haupo sasa. Basi, nenda ukale. Imani yako imetenda hilo, ndugu.

¹⁹⁴ Hebu tuseme, “Bwana asifiwe,” kila mtu. [Kusanyiko linasema, “Bwana asifiwe!”—Mh.] Yeye anabaki yule yule jana,

leo! Je! unaamini tunaweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya? [“Amina.”] Hakika, mnaamini!

¹⁹⁵ Je! unaamini hilo, dada? [Mwanamke huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Katika Jina la Yesu Kristo, nenda ukaponywe na ukawe mzima, kwa ajili ya—kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

¹⁹⁶ Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, pamoja na mambo yote yanayoendelea hapa katika jengo hili usiku wa leo, tunajua kwamba Wewe upo hapa. Jalia Nguvu za Mungu zimfanye dada yangu kuwa mzima, kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

¹⁹⁷ Njoo sasa, amini. Je, unaamini kwa moyo wako wote? [Mwanamke huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Haikupasi kulemaa basi. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aende na aponywe, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina. Nenda sasa, usitie shaka, amini kwa moyo wako wote.

¹⁹⁸ Moyo na tumbo pia; tumbo husababisha moyo. Bwana Yesu, mpe ndugu yangu afya. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

¹⁹⁹ Hivyo ndivyo tulikuwa tukifanya, muda mrefu uliopita, tukiomba, mwajua.

²⁰⁰ Sasa kwa kweli huna haja ya kuwa na wasiwasi, sivyo? Je! unayo? Si hata kidogo. Lakini una wasiwasi, hata hivyo. Hiyo ni kweli. Wote hao huko nje, karibu kila mmoja wao, analo jambo lile lile. Wanalo. Hebu niwaonyeshe.

²⁰¹ Ni wangapi walio na wasiwasi huko nje? Inueni mikono yenu. Inueni mikono yenu.

²⁰² Ungeitaje kundi hilo? Mnaona, usingeweza. Lakini hebu niwaonyeshe kwamba Mungu ndiye Mponya, maana ninajua unaenda kupona. Unaona? Kusema kweli, tayari imekwisha, sasa hivi. Hiyo ni kweli. Amina. Kivuli hicho kilimwondokea, papo hapo. Endelea, shangilia, na useme, “Asifiwe, Bwana!” Amina.

²⁰³ Hivi si ungetaka kupumua tena, vizuri? Na, naam, hiyo si ingekuwa ni ajabu? Je! unaamini anaweza? [Mwanamke huyo anasema, “Loo!”—Mh.] Basi nenda zako, na ufanye hivyo. Katika Jina la Yesu Kristo, na ifanyike. Amina.

²⁰⁴ Sasa unajua kwamba huna budi kupata usaidizi, au ufe. Itakuua usipopata usaidizi. Mungu yupo hapa kukusaidia. Je! unaamini hilo? Hebu nionyeshe jinsi kitu hicho kilivyo kiovu. Hebu nishike mkono wako hapa. Unajua, ilikuwa ni kansa. Je! ulijua ulikuwa na kansa? [Mwanamume huyo anasema, “Naam.”—Mh.] Je! utaamini kwa moyo wako wote, pamoja nami?

Mwanamume huyu hana budi kufa ikiwa Mungu hatamponya. Ilikuwa ni kansa.

205 Ee Mungu, Neno linasema, “Katika Jina Langu watatoa pepo.” Na kama umewafanyia wengine, Bwana Yesu, mfanyie mwanamume huyu hapa. Jalia Nguvu za Mungu Mwenyezi zije juu yake, na kuyaokoa maisha yake, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

206 Nenda na ukasahau hilo, useme tu, “Asante, Bwana,” na uende na ukaponywe kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

207 Sasa unahitaji upasuaji kwelikweli, hiyo ni kweli, wa kivimbe. Lakini Mungu, anayeweza kuondoa kivimbe kutoka kwa mke wangu, anaweza kukiondoa kwako. Je! unaamini hilo? Je! unaamini kwamba hadithi hiyo ni kweli, niliyosimulia muda mfupi uliopita? Huu hapa mkono wangu juu ya Biblia hapa, kwamba ni kweli. Sasa unajua Roho Mtakatifu yupo hapa. Sikujui, sijawahi kukuona. Na kama ninaweza kukuambia kuwa tatizo lako ni nini, haina budi kuwa ni Kitu fulani hapa kikiniambia. Vema, Kitu hicho hicho kiliondoa kivimbe kutoka kwa mke wangu, unaona. Sasa je! unaamini, kwa mimi kuomba tu na kukuwekea mikono, hicho kivimbe kitakuacha? Unaenda kuamini hilo kwa moyo wako wote? Vema, njoo hapa.

Nyinyi nyote aminini pamoja nami sasa.

208 Bwana Yesu, jalia neema Yako na rehema ziwe juu ya mwanamke huyu. Ninapoweka mikono juu yake, na katika msingi wa Neno la Mungu, jalia kivimbe hiki kikemewe, na hebu mwanamke huyu aishi kwa utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

209 Mungu akubariki sasa. Nenda, ukaamini, ukisema, “Asante, Bwana,” na chote kitakwisha.

210 Sasa ni kiasi gani cha...Tumepitiliza wakati kwa dakika tatu. Nimefaulu, kasoro dakika tatu. Nitakuwa sawa kesho usiku wa leo, Carl.

211 Ni wangapi wanampenda Bwana sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wanaamini kwamba watu hawa wameponywa? [“Amina!”] Kesho usiku nitajaribu kuichukua tofauti kidogo, na kuwaonyesha yote tena jinsi ambavyo hiyo hufanya kazi na jinsi inavyotumika, Bwana akipenda. Na sasa Bwana ambariki kila mmoja wenu.

212 Je! yupo mtu yeyote hapa aliyeshawishika kwamba wao ni mwenye dhambi, nao wanataka kumtumikia Yesu Kristo kama msaada wao, wamkubali Yesu kama Mwokozi wao? Je! ungetaka kusimama hapa sasa na kuturuhusu kuomba pamoja nawe? Tutafurahia kufanya hivyo. Mwaliko ni wazi, nasi tumeweka ibada hizi kwa ajili ya uponyaji, uponyaji wa Kiungu, bali si kwa uponyaji tu. Tunawaomba wagonjwa, na pia tuna...Wenye ugonjwa wa dhambi, hao ndio kwanza. Tunawatakeni mje. Na mje hapa kwa dakika moja, msimame pamoja nasi kwa maombi. Tutafurahia kuomba pamoja nanyi, tufanye yote tuwezayo ili kuwasaidia. Je! mtafanya hivyo? Je! yupo mwenye dhambi katika

jengo, angetaka kuchukua msimamo huo usiku wa leo, aseme, “Nitakuja na kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu binafsi. Ninataka kuokolewa, usiku wa leo?”

²¹³ Mungu akubariki. Huyu hapa anakuja mwanamume. Mungu akubariki. Je! kuna mwingine? Huenda kuna mwingine? Hivyo ndivyo ninavyopenda kuona watu wakija. Njoo moja kwa moja huku chini, wazi kabisa, na useme, “Niko makosani. Ninataka kuwa sawa.”

²¹⁴ Basi ndugu yangu, dada, mbele ya watu hawa mia tano mia sita, ama idadi yoyote iliyoko hapa ndani (Sijui), bali watu hawa wanaosimama hapa wanajua ni kweli. Kamwe Bwana hajawahi kuniacha niseme chochote kisicho kweli katika huo unabii. Ni wangapi wanasema, “Hiyo ni kweli”? Mnaoinua mikono yenu kama shahidi? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona, daima ni sahihi.

²¹⁵ Yeye atakuokoa ikiwa utakuja tu na imani rahisi, na kuamini. Yeye anajua siri ya moyo. Ni kwa nini nilifanya wito huo kwenye wakati huu tu, ilionekana kama kwamba jengo linavuma kwangu mimi? Ni kwa sababu Kitu fulani kilisema, “Fanya wito.” Nilijuaje kwamba hii huenda isiwe ni fursa ya mwisho kwa watu hawa? Huenda kukawa na wengine zaidi hapa. Kama wapo, mbona msije wakati tukiinamisha vichwa vyetu?

Njoo, bwana. Mungu akubariki. Hilo ni jema.

Bwana, mponye, mfanye mzima, na ulifanya hili—hili kwa ajili yake.

²¹⁶ Njoo, mtu mwingine? Watatu. “Katika kinywa cha mashahidi watatu, na liimarishwe.”

²¹⁷ Sasa, ndugu, wakati mnaposimama hapo, mnaofanya jambo la kishujaa sana. Watu walio wagonjwa, watafanya lolote ili wapate kupona. Bali wakati mtu anapotambua kwamba yu mgonjwa wa dhambi, huo ndio ugonjwa mbaya zaidi.

²¹⁸ Watu hawa wamekuja hapa usiku wa leo, ninajua kulikuwa na kansa kadhaa zilizoondoka tulipokuwa tumesimama hapa. Hiyo ni kweli. Niliona vivuli vikiondoka. Nami si shupavu wa dini. Ninajua ni kweli. Watu wengi waliponywa. Lakini huenda labda, wakati mwingine, wakiishi muda mrefu vya kutosha, watakuwa wagonjwa tena; huenda wakawa na nimonia. Kitu fulani hakina budi kuwaondoa maishani; kifo hakina budi kufanya hivyo.

²¹⁹ Sasa, lakini kile unachofanya sasa, unaenda kukubali Uzima wa Milele. Angalia yale Yesu aliyosema, “Yeye asikiaye Maneno Yangu.” *Asikiaye* maana yake ni “kuelewa.” Mnaona? “Yeye asikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele; wala hataingia hukumuni, bali amepita

kutoka mautini kuingia Uzimani.” Unafanya jambo la maana kuliko yote uliyowahi kufanya.

²²⁰ Nitaomba kusanyiko lisimame, katika kumbukumbu ya hili, wakati tukiomba. Baadhi ya wahudumu wangependa kuja karibu na kuweka mikono juu ya watu hawa, pamoja nami; na—na kuwa na furaha kwenu kufanya hivyo, kama mtafanya hivyo. Njoni papa hapa na mwawekee mikono yenu. Kila mtu kwa kicho.

²²¹ Baba wa Mbinguni, katika Uwepo Wako wa Kiungu; sio, chini ya mhemuko, bali chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, katika majira ya uponyaji wa Kiungu. Walipomwona Yesu akifanya mambo yaya haya, miaka elfu mbili iliyopita leo hii, nao wanamwona Yeye akiyafanya leo, wengi wanatenda kama walivyotenda wakati ule. Ilisema, “Wengi walimwamini Yeye, kwa sababu ya matendo Yake.” Wengi wanamwamini usiku wa leo, kwa sababu ya matendo Yake.

²²² Hapa zinasimama nafsi tatu za thamani, watu watatu. Inaonekana, Bwana, mara nyingi ni wanawake. Lakini usiku wa leo imekuwa ni wanaume, kote kote. Nasi tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba utapokea ma—maungamo yao, wanapokiri kwamba wamekuwa makosani, nao wanatamani kupata Uzima, na kuwa Nao tele, kupitia Yesu Kristo. Ondolea mbali kila doa jeusi la dhambi. Nisikie, Bwana, ninapooomba. Ninawakabidhi mikononi Mwako. Na kwa mamlaka ya Neno Lako, lililosema kwamba, “Yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe,” basi inakubidi Wewe kuwapokea, Bwana, kwa kuwa wamekuja, nalo Neno Lako lilisema kwamba usingewatupa nje. Nao wamekuja, wakiadini kwamba Wewe utawasamehe. Basi, kuanzia usiku wa leo na kuendelea, watakutumikia Wewe siku zao zote, wakijitenga na dhambi.

²²³ Ninaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba Wewe utamwaga Roho Mtakatifu juu yao, kwamba utawajaza na Nguvu Zako za Kiungu; kwamba wasiwe tu Wakristo, bali vyombo vya—vya huduma, waliojazwa kabisa, na Roho Mtakatifu, ili wasaidie kuleta Ujumbe kwa wengine.

²²⁴ Bwana Yesu, ninawakabidhi Kwako sasa, juu ya Neno Lako, lililoahidi kwamba “watasamehewa.” “Nitamfufua katika siku ya mwisho,” Wewe ulisema. Nami ninajua Maneno Yako ni kweli, tumekuwa tu tukiyezungumzia. Hayashindwi kamwe. Nalo Neno liliwajia watu hawa usiku wa leo, nao wamekuja kulifuata Neno. Tena ninajua, kwamba katika hii njia panda hapa, ya msamaha, kwamba Wewe unafanya hivyo, kwa kuwa Maneno Yako hayawezi kushindwa. Katika Jina la Yesu.

Huku vichwa vyetu vimeinamishwa sasa.

²²⁵ Kwenu nyinyi, ndugu zangu mnaosimama hapa usiku wa leo, mlifanya jambo la pekee mnaloweza kufanya. Unaposhawishika kwamba uko makosani, ndipo unashawishika kuwa na hatia ya

dhambi, kitu fulani ulichofanya makosa. Kuna njia moja tu ya msamaha, na hiyo ni kupitia Msalaba. Nanyi mmetembea mkaja hapa juu usiku wa leo, mbele ya watu hawa wote, kumkubali kama Mwokozi wenu, kwamba mlishawishika kwamba mko makosani, mna hatia; mkashawishika kwamba Yeye yu sahihi, mkashawishika kwamba mko makosani. Na Yeye alikufa kwa ajili ya wenye dhambi. Hiyo ndiyo iliyomleta, duniani, kufa kwa ajili ya wenye dhambi; akikuomba tu jambo moja, kukubali kwa hiari kile alichofia, kwa ajili yako. Je! utafanya hivyo, utampokea kama Mwokozi wako? Ziweke dhambi zako nyuma yako, na umkubali Yeye sasa hivi kama Mwokozi wako binafsi. Kama mtafanya hivyo, inueni tu mikono yenu ya kulia kumwelekea Yeye, "Nitafanya hivyo." Mungu awabariki.

²²⁶ Hiyo inamaanisha kwamba imekwisha! Kama mnaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu, basi hiyo ni kulingana na Neno Lake, "Dhambi zenu ziko nyuma yenu, zimeondoka. Ziko katika Bahari ya Usahaulifu, Yeye hatazikumbuka tena. Ninyi ni viumbe vipya katika Yeye, usiku wa leo." Sasa naomba . . .

²²⁷ Ndugu hawa hapa watakuja na kuwawekea mikono. Na baadhi yenu wahudumu hapa simameni karibu, njoni, wekeni mikono yenu, pia, na hebu tuwabariki, ili wapokee Roho Mtakatifu. Njoni karibu.

²²⁸ Baba wa Mbinguni, mjaze huyu ndugu mzuri na...?... Mjaze huyu, ndugu yangu, kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mjaze huyu, ndugu yangu, Bwana, usiku wa leo, na Roho Mtakatifu. Tujalie haya, katika Jina la Yesu Kristo, ninapowakabidhi Kwako, kwa ajili ya watumishi Wako. Amina.

²²⁹ Sasa mwaweza kuinua vichwa vyenu. Watu hawa wamemkubali Kristo kama Mwokozi wao; dhambi za kale zimesamehewa. Hilo ni Neno la Bwana. Ni wangapi wanajua hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

²³⁰ Sasa ninawatakeni mgeuke kuelekea wasikilizaji, enyi marafiki. Kwa hiyo Yeye anasema, "Mkinionea haya mbele ya wanadamu, Mimi ninawaonea haya mbele ya Baba. Yeye atakayenikiri Mimi mbele ya wanadamu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu." Inueni mikono yenu, kwamba mnakiri kwamba Yesu Kristo ni Mwokozi wenu, mnamchukua kuwa Mwokozi wenu sasa. Nyinyi ndugu hapa inueni, mliokuja mimbarani hivi sasa, inueni mikono yenu, ili wasikilizaji waweze kuona. "Yeye anayenikiri Mimi mbele ya wanadamu, huyo nitamkiri mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu."

Sasa tunapoinamisha vichwa vyetu, kwa ajili ya kufumukana.

²³¹ Ninataka kila mmoja wenu, wale wanaoweza, mje hapa karibu na kupeana mikono na ndugu hawa. Na muwaalike

kanisani mwenu, baadhi yenu wachungaji, ili mwendelee pamoja nao, kuanzia hapa, kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

²³² Mungu awabariki. Mungu awaponye. Mungu awape neema, kwa wingi, ndiyo maombi yangu manyenyekevu. Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa wakati, nadhani, Ndugu Rose anakuja kwa ajili ya maombi ya kufumukana. Vema, Ndugu Rose.



MANENO YAKE YA AHADI YASIYOSHINDWA SWA64-0120

(His Unfailing Words Of Promise)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, tarehe 20 Januari, 1964, katika Hoteli ya Ramada kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org